JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## MATOKEO YA MNADA WA MASAFA KATIKA BENDI YA 3600-3800 MHz KWA AJILI YA MAWASILIANO YA SIMU NA INTANETI

Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 na Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 ya Sheria za Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ina jukumu la kupanga, kuidhinisha, kugawa, kutoa, kuchukua, kusimamisha matumizi, kufuta au kwa namna yoyote ile kurekebisha mgawanyo wa masafa miongoni mwa watumiaji au wenye leseni za masafa ya mawasiliano.

Katika kutekeleza majukumu yake, tarehe 18 Desemba 2024, TCRA ilitoa taarifa kwa Umma kuhusu mpango wa ugawaji wa masafa katika Bendi ya 3600 - 3800 MHz kwa njia ya mnada, yatakayotumika kwa ajili ya mawasiliano ya simu na intaneti. Mnada huu umezingatia Sheria za nchi pamoja na Kanuni na Miongozo ya Shirika la Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union – ITU). Mchakato wa mnada wa ugawaji wa masafa pamoja na masuala mengine ulijumuisha, Tathmini ya Kiufundi na Hali ya Soko iliyofuatiwa na ushirikishwaji wa wadau uliokamilika tarehe 21 Mei 2025. Tarehe 02 Juni 2025, TCRA ilichapisha Waraka wa Taarifa ya Mnada (Information Memorandum). Aidha, tarehe 10 Julai 2025, TCRA ilihitimisha ugawaji wa masafa katika Bendi ya 3600 - 3800 MHz kwa njia ya Mnada.

Mnada huu umezingatia malengo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016, katika matumizi ya masafa ya mawasiliano yenye faida zifuatazo:

(a) Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijiti (2024-2034) kwa kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ya kasi ili kuchochea maendeleo ya uchumi wa kidijiti katika sekta zote ikiwemo uchumi wa buluu;

(b) Uwezeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kama vile elimu, afya, kilimo, biashara na huduma za kifedha;

(c) Kuimarisha ubora wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji;

(d) Kuongeza usambazaji wa huduma za mawasiliano ya kasi kwa wananchi wengi zaidi; na

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz

(e) Kuendeleza na kuwezesha ubunifu wa huduma mpya zinazowezeshwa na TEHAMA, teknolojia ya 5G na teknolojia nyingine za mawasiliano ya simu na intaneti zinazoibukia.

TCRA inapenda kutoa taarifa kwa Umma kuhusu matokeo ya mnada huu uliofanyika kwa mafanikio tarehe 10 Julai 2025 kwa kugawa vitalu vyote vinne (4) vilivyo kuwepo. Watoa huduma za mawasiliano watatu (3) walishiriki na wote wameshinda na kupata masafa katika Bendi ya 3600 - 3800 MHz kwa idadi ya vitalu kama inavyoonekana katika jedwali:

| Na | Mtoa Huduma | Idadi ya Vitalu | Kiasi Kitakacholipwa (TZS) |
|---|---|---|---|
| **1** | Viettel Tanzania Plc (Halotel) | 2 | 130,439,999,999.98 |
| **2** | Honora Tanzania Plc (Yas) | 1 | 55,500,000,000.00 |
| **3** | Vodacom Tanzania Plc | 1 | 49,768,986,876.89 |
| Jumla ya kiasi kitakacholipwa (TZS) | | | 235,708,986,876.87 |

Malipo ya masafa katika mnada huu yatafanyika kwa awamu tano (5) kwa kipindi cha miaka miwili (2) kuanzia tarehe ya mnada hadi mwaka 2027 kwa mujibu wa Waraka wa Taarifa ya Mnada (Information Memorandum). Awamu hizi za malipo zina lengo la kuwawezesha washindi wa mnada huu kuwekeza kwa ufanisi katika miundombinu ya mawasiliano ya simu na intaneti ili kufikia malengo yanayotarajiwa katika matumizi ya masafa haya (3600 - 3800 MHz).

CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

TCRA inazipongeza kampuni za Viettel Tanzania Plc, Honora Tanzania Plc and Vodacom Tanzania Plc kwa kushinda na kupata masafa katika Bendi ya 3600 - 3800 MHz.

Imetolewa Tarehe **10 Julai, 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Thu Jul 10 16:44:01 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**